


# Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 02 Issue: 01 | Jan-2023

EAJK


# Maoni ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuhusu nafasi ya Kiswahili katika elimu ya ufundi nchini Kenya


**Author**

**Jackson Mutuku Kavoi**

**Email: mutukukavoi@yahoo.com**

**Kabarak University, Kenya**



**Cite this article in APA**

Kavoi, J. M. (2023). Maoni ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuhusu nafasi ya Kiswahili katika elimu ya ufundi nchini Kenya. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 2*(1), 84-94. https://doi.org/10.51317/eajk.v2i1.329

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**

Received: 20.10.2022

Accepted: 15.1.2023

Published: 19.1.2023

Scan this QR to read the paper online



**Copyright**: ©2023 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY) and their terms and conditions.



**Ikisiri**

Utafiti huu ulinuia kutafuta maoni ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuhusu nafasi ya lugha ya Kiswahili katika elimu ya kiufundi. Muundo wa Uchunguzi Kimaelezo ulitumiwa, huku taasisi 5 za kiufundi za kitaifa na sampuli ya wanafunzi 148 na wakufunzi 20 wakishirikishwa katika utafiti. Aidha, utafiti huu ulitumia hojaji na mahojiano kukusanya data. Mbinu ya Yaliyomo Mchanganuo ilitumiwa kuchanganua data. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili huchukua nafasi kuu katika mtaala wa elimu ya ufundi katika taasisi za kiufundi za kitaifa nchini. Kwa sasa, Kiswahili sio lugha ya ufundishaji katika taasisi hizi, ila hutumiwa na wakufunzi wa kozi mbalimbali kudadavua dhana tata, hasa miongoni mwa wanafunzi wa astashahada. Pia, utafiti huu zaidi uligundua kuwa Kiswahili ni lugha ya mawasiliano kwa wanafunzi wengi. Kutokana na majukumu haya yaliyodokezwa na wasailiwa, utafiti unapendekeza kwa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayanzi na Teknolojia (MOHEST), ikishirikiana Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (KICD) kubuni mkakati wa kuanzisha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kama somo katika taasisi za ufundi nchini. Kwa kufanya hivyo, taasisi tajwa zitakuwa zikihimilisha dhima za kiakademia na kijamii ambazo hutekelezwa na Kiswahili katika mtaala wa elimu ya ufundi. Utafiti zaidi unaweza kulinganisha na kulinganua mielekeo ya wanafunzi wa taasisi za ufundi kuhusu Kiswahili na Kiingereza kama lugha ya kutoa mafunzo miongoni mwa wanafunzi wa astashahada.



**Maneno muhimu:** Astashahada, elimu ya kiufundi, maoni ya wanafunzi, stashahada, taasisi za ufundi za kitaifa.

**UTANGULIZI**

Massamba na Wenzake (2001) wanafafanua lugha kama mfumo wa sauti nasibu ambazo hutumiwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao. Kimsingi katika lugha sahili kabisa dhana ya lugha inaweza kufafanuliwa kama mfumo wa sauti nasibu unaotumiwa na jamii mahsusi kwa ajili ya mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Trudgil (1974) anasema "lugha inaweza kuwa jambo la muhimu katika … kutambulisha kundi … pia inaweza kuathiri jamii au hata kutumika kudhibiti muonoulimwengu wa wazungumzaji" (uk. 24). Kutokana na uelewa huu, tunaweza kuhitimisha kuwa lugha ni chombo muhimu katika kushajiisha maendeleo miongoni mwa wazungumzaji wa lugha husika (Ipara & Mbori, 2009). Kwa mkabala huu, ikiwa lugha inaweza kutumiwa kuhawilisha maarifa, basi Kiswahili, kama mojawapo ya lugha ya kimataifa yenye wazungumzaji zaidi ya milioni 100 katika bara la Afrika, haiwezi kupuuzika (Payne, 2014). Zaidi ya haya, Payne anaendelea kusema kuwa, Kiswahili ni lugha inayotumika katika biashara, lugha ya taifa nchini Kenya, Tanzania, Uganda na DRC, lugha ya matangamano ya biashara barani Afrika inayohusishwa na teknolojia ya mawasiliano, Sanaa na utamaduni, lingua franka na pia kutumika katika mashirika ya kutajika ya mawasiliano kama BBC, VOA na Deutsche Welle. Aidha, Kiswahili ni chombo cha mawasiliano na pia ishara ya utambulisho kikanda na muungano wa watu wa Afrika Mashariki, pamoja na utamaduni wao (Habwe, 2018). Kando na haya, kwa mujibu wa Webb na Kembo-Sure (2000), lugha ya Kiswahili ina wazungumzaji wazawa zaidi ya milioni tano.

Tangu enzi ya ukoloni lugha ya Kiingereza imekuwa na hadhi ya juu ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili. Licha ya lugha ya Kiswahili kuwa na wazungumzaji zaidi ya asilimia 80 nchini Kenya ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza ambayo ina wazungumzaji chini ya asilimia 20, hadhi yake imekuwa ya chini. Hii inaweza kuwa ndio sababu lugha ya Kiingereza na Stadi za Mawasiliano kwa Kiingereza hufundishwa katika takriban taasisi za juu za elimu pamoja na taasisi za ufundi za kitaifa nchini. Vilevile, lugha ya Kiingereza imekuwa ndiyo lugha rasmi nchini Kenya hadi kuzinduliwa kwa katiba mpya mwaka 2010 ambapo lugha ya Kiswahili nayo ikatangazwa kuwa lugha rasmi. Hata hivyo, jukumu hili ambalo lugha ya Kiswahili ilitwikwa na katiba mpya haijashika mizizi katika ofisi nyingi za umma katika kaunti ya Kisii (Nyandwaro, 2015). Kiuhalisia, hili ndilo linalotukia kwa maafisa wengi wa umma kuonekana kupigia upatu matumizi ya lugha ya Kiswahili, jambo ambalo ni kinyume na kinachotukia kiuhalisia. Hata hivyo, wazungumzaji wa Kiswahili wangali mbioni katika harakati za kuimarisha lugha ya Kiswahili.

Fauka ya haya, lugha ya Kiswahili ilikuwa ikipiga hatua tatu na kurudi nyuma hatua mbili katika elimu ya kiufundi, hususan miaka ya 1990 somo la Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili lilikuwa likifundishwa wanafunzi wa kiwango cha astashahada katika taasisi za ufundi, ila baadaye likaondolewa bila kusema sababu za kuliondoa. Hata hivyo, afisa elimu ufundi alipokuwa akiohojiwa na mtafiti, alidokeza kuwa Wizara ya Elimu ilionelea somo la Stadi za Mawasiliano kwa Kiingereza waliona lilikuwa likiwahudumia wanafunzi husika bila tatizo lolote. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili ilipata msukumo kwa sababu ilibakia ikifundishwa wanafunzi wa kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii (Uwandani, 2019). Hivyo, hii ni dhihirisho tosha kuwa lugha ya Kiswahili ina jukumu katika ustawi wa jamii na elimu miongoni mwa wanafunzi wa taasisi za kiufundi. Kimsingi, ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu uliendeshwa ili kubainisha maoni ya wanafunzi wa taasisi za ufundi za kitaifa kuhusu dhima ya lugha ya Kiswahili katika elimu ya ufundi kwa sababu wao ni washika dau katika suala nzima.

Kimsingi, lugha ya Kiswahili hufahamika kwa asilimia ya juu ya watu nchini, na hufanya msingi kabambe wa mawasiliano katika kuendesha masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hufundishwa katika kiwango cha shule za msingi, sekondari na chuo kikuu. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili japo hufundishwa katika kiwango cha astashahada katika taasisi za kiufundi za kitaifa haitiniwi na haishirikishwa katika mtaala wa elimu ya taasisi husika. Swali kuwa lugha Kiswahili japo haijashirikishwa katika mtaala wa elimu wa taasisi hizi haina nafasi yoyote kwa walengwa? Utafiti huu unalenga kuchunguza maoni ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuhusu nafasi ya Kiswahili katika elimu ya taasisi husika.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Kwa ujumla, wataalamu mbalimbali wa Kiswahili wana maoni kuwa, nafasi ya Kiswahili ni pana sana kwa

sababu hutumika kama lugha ya kitaifa na kimataifa. Kwa mfano, Kihore (1983), Kiango (2002) na Kandagor (2014) wana maoni kuwa Kiswahili ni lugha ambayo huunganisha mataifa ya Afrika ya kati na mashariki. Kuhusu muungano huu, Keiko (2014) anasema kuwa Kiswahili kina nafasi ya kuunganisha kielimu taifa la Japan na mataifa ya Afrika Mashariki katika siku za usoni.

Kwa mujibu wa Kihore (1983) na Kiango (2002), Kiswahili ni lugha ya kufundishia katika taasisi za elimu nchini Tanzania na ni somo la lazima katika kiwango cha shule za msingi na upili na hufundishwa katika vyuo vikuu katika mataifa ya Kenya na Tanzania. Makala za wasomi hawa, akina Kihore (1983), Kiango (2002), Kandagor (2014) na Keiko (2014) zinadhihirisha umuhimu wa Kiswahili kama kiunganishi cha mataifa mbalimbali; maandishi ambayo yana umuhimu katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu yanatoa mwanga kuhusu nafasi ya Kiswahili katika kuleta muungano mingoni mwa mataifa mbalimbali kwa upande wa kisiasa, kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa sababu unachangia kutafuta nafasi ya Kiswahili katika elimu ya taasisi za kiufundi za kitaifa.

Vivyo hivyo, kwa maoni ya Mukuthuria (2006), nchini Uganda, kuna kauli ya kisiasa kuwa Kiswahili kinapaswa kuwa somo la lazima katika shule za msingi na za upili, japo kauli hii bado haijafanyiwa kazi. Hata hivyo, Kiswahili ni mojawapo ya masomo yanayofundishwa katika vyuo vikuu vya Kyambogo, Makerere na Chuo Kikuu cha Kiislamu, Mbale. Pia, Kiswahili ni lugha ya pili rasmi kupitia sheria ya mbunge tangu 2005 na hutumika katika vituo vya redio, hususani OPG FM, Mbale FM na redio ya kitaifa nchini Uganda. Hali ya Kiswahili inaendelea kubadilika kila kukicha na mielekeo ya Waganda inaendelea kubadilika kutoka lugha ya utawala wa kibabe hadi lugha ya kuendesha biashara. Waganda tayari wameshaagundua kuwa ili waweze kushiriki katika shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi Afrika Mashariki hawana bundi kukaribisha Kiswahili katika nyanja tofautitofauti. Maoni ya msomi huyu yanadhihirisha hali ya Kiswahili ilivyo nchini Uganda katika nyanja tofautitofauti, hususan elimu, dini, biashara na siasa. Makala hii ni muhimu kwa utafiti shughulikiwa kwasababu inatuingiza katika kupambanua umuhimu wa Kiswahili nchini Uganda; nchi ambayo watu wake miaka michache iliyopita walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Kwa sasa, rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni anapotembelea mataifa jirani ya Afrika Mashariki uhuhakikisha anatoa hotuba zake kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni ishara nzuri kuwa mielekeo ya Waganda kuhusu lugha ya Kiswahili inaendelea kubadilika. Utafiti wa Mukuthuria ulichangia kuelezea hali ya Kiswahili ilivyo na matumizi yake nchini Uganda. Tofauti naye, utafiti huu unatafuta nafasi ya Kiswahili katika elimu ya taasisi za kiufundi za taifa nchini Kenya.

Mbali na Kiswahili kuwa kivuko cha muungano katika mataifa ya Afrika Mashariki, kwa mujibu wa Kandagor (2014), Kiswahili kinaweza kutumika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI. Pia, Mwaliwa (2014), ana maoni kuwa Kiswahili kina nafasi nzuri katika utangazaji katika redio na runinga nchini Kenya mtawalia. Hata hivyo, anaendelea kusema kuwa baadhi ya vipindi vya runinga, vina matumizi mengi ya *Sheng'* ikilinganishwa na Kiswahili sanifu. Hali hii, anasema imechangia kuboronga Kiswahili katika sekta ya elimu. Hata hivyo, matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali hushuhudiwa miongoni mwa jamii tofautitofauti. Hata hivyo, baadhi ya maneno yanayotumika katika vipindi hivi baadaye hupitwa na wakati na kutotumika tena na uborongaji husika hufifia.

Mbali na Kiswahili kuwa na nafasi nzuri ya kuunganisha mataifa ya Afrika Mashariki, Kalindimya (2004) aliona tishio kubwa ya kukwamisha juhudi hizi ni utandawazi. Hivyo, mataifa yenye uwezo mkubwa na nyenzo mbalimbali za kuendeleza lugha zao yalikuwa yakiendelea kukwamisha juhudi za Kiswahili kuwa lugha ya ufundishaji katika mataifa yanayokimiliki. Anasema kuwa kinachosababisha hali hii ni mataifa haya kuwa na ushirika na vibaraka katika mataifa ya Afrika Mashariki. Vibaraka hawa na marafiki zao wangali wanaona Kiswahili hakijafikia hatua ya kutumika kama lugha ya ufundishaji.

Senkoro (2005) katika utafiti wake uliofadhiliwa na COSEDERIA na kuhusisha walimu, wanafunzi na wazazi, nchini Tanzania, ulilenga kubainisha iwapo lugha ya Kiswahili ingeweza kutumiwa kama lugha fundishi katika kiwango cha shule za sekondari. Matokeo yake yalikuwa si ya kuridhisha. Hii ni kwa sababu licha ya walimu na wanafunzi kutokifahamu Kiingereza, walikiunga mkono kiendelee kutumika kama lugha ya ufundishaji. Matokeo ya utafiti wake

yalidhihirisha kuwa, wanafunzi waliona ikiwa Kiswahili kingetumika kama lugha ya kufundishia wangeachwa nyuma kimawasiliano na kiteknolojia. Hivyo, mkatiko wa mawasiliano ungedhihirika baina ya nchi yao na ulimwengu mpana na wangebakia nyuma kimaendeleo. Kwa upande wa walimu na wazazi, walikuwa na imani kuwa watoto wao wakifundishwa kwa Kiingereza walikuwa wamepata elimu bora. Kwao, ilikuwa ni heri wanafunzi kufundishwa kwa Kiingereza kibovu kuliko kufundishwa kwa Kiswahili. Utafiti wa Senkoro (2005) una mashiko kwa sababu kufikia sasa wazazi wenye uwezo kifedha hukazania kuwapeleka watoto wao katika shule za msingi za kibinafsi ambazo hutumia lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia. Shule hizi zimekuja kujulikana kama *English Medium Schools*. Vilevile, wazazi wenye kujipata zaidi kiuchumi hupeleka watoto wao nchini Kenya kwa sababu wanaamini wangejifunza angalao Kiingereza ambacho wanakinasibisha na elimu bora.

Utafiti wa Senkoro (2005) ni wa umuhimu mkubwa kwa sababu unatufunua macho kuhusu nafasi ya Kiswahili katika elimu ya Tanzania na mitazamo ya wanafunzi, walimu na wazazi kuhusu Kiswahili kama lugha ya kufundishia. Utafiti uliofanywa na Senkoro ulikuwa unatafuta nafasi ya Kiswahili katika elimu ya Tanzania kama lugha ya kufundishia, ilhali wetu unabainisha nafasi ya Kiswahili katika elimu ya taasisi za kiufundi za kitaifa. Hii ni kwa sababu mafuzu wa taasisi husika hulazimika kutoa huduma kwa Kiswahili wanapohitimu na kutumwa nyanjani kuwahudumia wananchi.

**MATOKEO**


Utafiti huu, kwa ujumla, ulishirikisha wasailiwa 148, hata hivyo ni 142 walizingatiwa katika uchanganuzi wa data. Wasailiwa hawa walijumuisha wanafunzi wa michepuo ya sayansi na Sanaa kutoka taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya. Wasailiwa kutoka mchepuo wa Sanaa walikuwa asilimia 48.59 (n=69) na sayansi asilimia 51.41 (n=73). Wasailiwa walikuwa na umri wa katikati ya miaka chini ya (<) 20 na zaidi ya (>) 35. Wasailiwa wengi walikuwa katika umri wa miaka kati ya 20 hadi miaka 25; wote wakiwa asilimia 77 (n=107). Waliokuwa chini ya miaka 20 walikuwa asilimia 14 (n=20), ilhali waliokuwa katika umri wa miaka 26 hadi 30 walikuwa asilimia 7 (n=10); 35 hadi 35 na chini ya miaka 35 walikuwa asilimia 1 (n=1) mtawalia. Msambao huu unadhihirishwa katika jedwali la 1 chini.

**Jedwali 1: Sifa za Kidemografia za Wanafunzi wa Taasisi za Kiufundi za Kitaifa**

| Sifa (Umri, Michepuo, Madaraja) | Idadi ya Wasailiwa (n) | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| **Umri** | | |
| < 20 | 20 | 14 |
| 20-25 | 107 | 77 |
| 26-30 | 10 | 7 |
| 31-35 | 1 | 1 |
| >35 | 1 | 1 |
| **Michepuo** | | |
| Sanaa | 69 | 48.59 |
| Sayansi | 73 | 51.41 |

Chanzo: Uwandani, 2017

Jedwali 1 inawasilisha sifa za kidemografia za wasailiwa walioshiriki katika utafiti huu. Jedwali hili limezalishwa kutoka kozi zilizo na mketo wa utoaji huduma ambazo ziliteuliwa kimakusudi. Wasailiwa hawa walitolewa kutoka michepuo ya Sanaa na Sayansi. Data husika inaonesha wazi kuwa wasailiwa wengi walitoka katika mchepuo wa sayansi (51.41%) ikilinganishwa na mchepuo wa sanaa (48.59%). Hii ni kwa sababu mara nyingi wanafunzi wa sayansi katika taasisi za kiufundi huwa ndio wengi. Kwa upande wa umri, wasailiwa takriban walikuwa vijana katikati ya miaka 20 na 25. Kozi zilizotumika katika utafiti huu ni zile zilizokuwa zikibobea upande wa utoaji huduma inavyodhihirishwa na kielelezo 1 kifuatacho.




**Kielelezo 1: Msambao wa Kozi Teule Kiasilimia (%) kwa Kuzingatia Kigezo cha Utoaji Huduma**

Chanzo: Uwandani, 2017

Kielelezo 1 juu kinaangazia msambao wa kozi teule kwa kuzingatia kigezo cha utoaji wa huduma. Kozi husika ni pamoja na: Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii ikiwa na asilimia 21.83 (n=); ikifuatwa kwa ukaribu na kozi ya Ufundi wa Umeme (19.72). Kozi nyingine zenye wasailiwa kiasi, zilikuwa ni pamoja na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika yenye asilimia 14.08 (n=20) na Teknolojia ya Vipimo vya Matibabu ikiwa na asilimia 11.27 (n=16). Hizi na nyingine zenye idadi wastani zilikuwa ni pamoja na Usimamizi wa Msururu wa Usambazaji, asilimia 8.4 (n=12) na Kilimo cha Kawaida asilimia 9.86 (n=14). Kozi ambazo zilishirikisha idadi ndogo ya wasailiwa zilikuwa ni pamoja na Usimamizi wa Biashara, asilimia 2.82 (n=4); Mauzo na Masoko, asilimia 2.11 (n=3); Ununuzi na Usambazaji, asilimia 1.41 (n=2) na Usimamizi wa Wafanyakazi, asilimia 1.41 (n=2) kwa upande wa sanaa. Kwa upande wa sayansi, kozi wakilishi zenye wasailiwa wachache zilikuwa ni Teknolojia Sayansi ya Maabara, asilimia 4.23 (n=6); Mitindo ya Nguo na Ushonaji, asilimia 1.41 (n=2) na Ususi na Tiba ya Urembo, asilimia 1.41 (n=2). Hivyo, kozi 13 (7 za sanaa na 6 za sayansi zenye mketo huduma) zilitumika katika utafiti huu zikiwa zimeteuliwa kimakusudi kama koza za utoaji wa huduma. Kwa hali hii, idadi ya wasailiwa ilienda kwa kiwango sawa na idadi ya wanafunzi katika taasisi za kiufundi za kitaifa. Ni wazi kuwa kutokana data hii, baadhi ya kozi zinatia fora zaidi ya nyingine. Kwa mfano, kozi za Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii (21.83%), Ufundi wa Umeme (19.72%), Usimamizi wa vyama vya Ushirika (14.08%) na Teknolojia ya Vipimo vya Matibabu (11.27%).

**Maoni ya Wanafunzi kuhusu Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili kwa Elimu ya Kiufundi**

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza maoni ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuhusu nafasi ya lugha ya Kiswahili katika elimu ya kiufundi. Ili kufikia lengo hili, utafiti husika ulitarajiwa kujibu swali "Wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa

wanaofanya kozi mbalimbali wana maoni yapi kuhusu nafasi ya lugha ya Kiswahili kwa elimu ya kiufundi?" Ili kushughulikia swali hili, miitikio ya wasailiwa ambao walikuwa wanfunzi wa taasisi husika ilichanganuliwa kupitia mbinu ya Uchanganuzi Yaliyomo. Kutokana na matokeo ya uchanganuzi husika, ilihitimishwa kuwa, lugha ya Kiswahili ilikuwa muhimu katika uendeshaji wa masuala mbalimbali katika taasisi hizi ambayo hayakuwa yameshirikishwa katika mtaala wa mafunzo. Pembeni, lugha ya Kiswahili iligunduliwa ilikuwa ikitumika kufafanua istilahi gumu kwa wanafunzi, chombo cha uelekezaji na ushauri, lugha ya utoaji huduma, mijadala ya kiakademia, lugha ya mawasiliano baina ya wanafunzi na wafanyakazi mhimili na pia somo kwa wanafunzi wanaosoma kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii katika kiwango cha astashahada. Aidha, wasailiwa waliombwa kutaja lugha ambayo ilikuwa ikitumika katika maeneo mbalimbali katika taasisi husika. Maeneo haya yalikuwa ni pamoja na maofisini, vikaoni, mabango ya matangazo, hotuba za mkuu wa chuo na katika shughuli za michezo katika nyanja tofautitofauti. Jedwali 2 lifuatalo linaonesha lugha ambayo hutumika katika maeneo mbalimbali katika taasisi za kiufundi za kitaifa.

**Jedwali 2: Lugha-Mawasiliano katika Maeneo Mbalimbali ya Taasisi za Kiufundi**

| Eneo la matumizi | Lugha-mawasiliano katika maeneo mbalimbali katika (%) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiingereza | | Kiswahili | | Jumla | |
| | Ut | % | Ut | % | Ut | % |
| Ofisini | 166 | 82.86 | 24 | 17.14 | 140 | 100 |
| Mikutanoni | 105 | 75.00 | 35 | 25 | 140 | 100 |
| Mabangoni | 89 | 64.03 | 50 | 35.97 | 139 | 100 |
| Hotuba za mkuu wa taasisi | 113 | 81.88 | 25 | 18.12 | 138 | 100 |
| Michezoni | 27 | 19.42 | 112 | 80.58 | 139 | 100 |

Chanzo: Uwandani, 2017

Kutokana na jedwali 2 iliyo juu, inaweza kugundulika kuwa lugha zinazotumika kwa wingi katika taasisi za kiufundi ni Kiingereza na Kiswahili na matumizi yake yanaweza kudhihirika kuwili: rasmi na yasiyo rasmi. Ni wazi kuwa, kutokana na takwimu Kiingereza hutumika katika masuala rasmi yanayogusia ofisi, vikao, mabango, hotuba za mkuu wa chuo wakati wa mikutano, ilhali Kiswahili hutumika katika masuala yasiyo ya kiofisi hususan, shughuli za michezo. Japokuwa lugha ya Kiswahili ilitangazwa kuwa lugha rasmi wakati wa kuzindua katiba mpya 2010, Kiingereza kimebakia kuwa ndiyo lugha kuu katika masuala rasmi. Idhibati ni kuwa asilimia 82.86 (n=116) ya wasailiwa walisema kuwa lugha iliyokuwa ikitumika maofisini ilikuwa lugha ya Kiingereza, ilhali asilimia 17.14 (n=24) walisema ni lugha ya Kiswahili. Katika vikao asilimia 75 (n=105), mabango asilimia 64.03(n=89), na hotuba za mkuu wa chuo mikutanoni asilimia 81.88 (n=113), ilihali matumizi ya lugha ya Kiswahili katika maeneo yayo hayo ilikuwa asilimia 25 (n=35), 35.97 (n=50), 18.12 (n=25), 80.58 (n=112) mtawalia. Kutokana na matokeo haya, ni wazi kuwa lugha ya Kiingereza ilitumika kwa mapana katika masuala rasmi tofauti na lugha ya Kiswahili iliyotumika katika masuala yasiyo rasmi kama wakati wanafunzi walipokuwa wakishangilia na katika kuendesha michezo husika. Matokeo ya utafiti huu yanalandana na ya utafiti wa Nyandwaro (2015) ambao uligundua kuwa licha ya lugha ya Kiswahili kutangazwa kuwa lugha rasmi ya kwanza, lugha ya Kiingereza ilibakia kuwa lugha rasmi katika ofisi nyingi za Kaunti ya Kisii.

Licha ya lugha ya Kiswahili kutumika katika eneo la michezo, iligundulika kuwa ilikuwa na majukumu

mengine yaliyokuwa yakibobea zaidi mtaala wa taasisi za kiufundi za kitaifa na masuala mengine ambayo hayakuwa yakilenga mtaala. Majukumu haya yamewasilishwa katika jedwali la 3 lifuatalo yakifuatana kwa umuhimu.

**Jedwali 3: Nafasi Zaidi ya Lugha ya Kiswahili katika Elimu ya Taasisi za Kiufundi za Kitaifa**

| Nafasi zaidi za lugha ya Kiswahili | Umaratokezi (ƒ) | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Ufafanuzi wa dhana | 38 | 27.14 |
| Ushauri nasaha | 29 | 20.71 |
| Huduma uwandani | 22 | 15.71 |
| Somo mhimili kwa kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii | 15 | 10.71 |
| Mikutano isiyo rasmi | 9 | 6.43 |
| Mazungumzo na wafanyakazi mhimili | 7 | 5.00 |
| Mahubiri | 6 | 4.29 |
| Mijadala ya kiakademia | 4 | 2.86 |
| Mazungumzo na wahadhiri | 2 | 1.43 |
| Mawasiliano katika simu | 2 | 1.43 |
| Haina nafasi yoyote | 6 | 4.29 |
| **Jumla** | **140** | **100.00** |

Chanzo: Uwandani, 2017

Kutokana na matokeo yanayowasilishwa katika jedwali la 3, majukumu yanayotekelezwa na lugha ya Kiswahili katika taasisi za kiufundi za kitaifa yameorodheshwa yakizingatia umuhimu kama walivyosema wasailiwa. Majukumu yanayolenga mtaala wa mafunzo ni pamoja na ufafanuzi wa dhana gumu (27.14 %,n=38); ushauri nasaha (20.71%,n=29); utoaji wa huduma (15.71%, n=22); ufundishaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii (10.71%, n=15); mijadala ya kiakademia (2.86%, n=4) wakati wa maandalizi ya mitihani ya ndani na ya kitaifa.

Fauka ya haya, inaweza kuhitimishwa kuwa asilimia 27.14 (n=38) ya wasailiwa ilisema kuwa wahadhiri walitumia lugha ya Kiswahili mara nyingi kufafanua istilahi zilizokuwa nje ya fikira za wanafunzi. Inasemekana, kama ilivyodokezwa na wahadhiri, wanafunzi katikati ya muhadhara wangemuuliza mhadhiri kwa lugha ya Kiswahili afafanue zaidi alichokuwa akiwasilisha. Vivyo hivyo, wahadhiri wangetumia lugha ya Kiswahili ili kupambanua dhana tata. Matumizi ya Kiswahili kuweka wazi dhana mbalimbali sio jambo geni kwa sababu inadhihirisha kuna kitu kinachokosekana katika mfumo mzima ili ifikie ukamilifu katika utendakazi wake kama wanauamilifu wasemavyo. Kushadidia haya, Biton et al. (2002) wanasema "uzima wa kiumbe chochote kile hutegemea viungo vinavyounda mfumo mzima na kuufanya kuwa unafanya kazi pamoja; kila kiungo kikifanya kazi ili kukamilisha uzima wa kiumbe husika, k.v mwili" (uk. 471). Maoni ya wanauamilifu yanaweza kutumika katika hali ya Kenya kwa sababu wakati

wahadhiri wanahamisha msimbo kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, huwa ni kwa manufaa ya somo na dhana mbalimbali kueleweka na wanafunzi. Kwa mkabala huu, kama ilivyo kwa kiumbe chenye uhai viungo vyote hutegemeana ili utimilifu na ukamilifu wa jukumu fulani ufikiwe na ufaulu wake udhihirike (Eshleman et al., 1993). Kwa hali hii, haya yanaweza kudhihirika katika somo kwa kutumia Kiswahili ambapo somo husika linahimilishwa na ukamilifu wake kufikiwa.

Ijapokuwa lugha ya Kiswahili sio lugha ya ufundishaji katika taasisi za kiufundi za kitaifa, huwasaidia wanafunzi katika mchakato wa ubunaji wa mawazo. Ipara na Mbori (2009) wanasema "Lugha ni kiwakilishi cha ishara cha uamilifu … na hatimaye, huamua fikira na muelekeo wa mtu" (uk.144). Kwa mkabala huu, wanafunzi wa astashahada wa taasisi tafitiwa hubuni mawazo yao kwa lugha ya Kiswahili na huyahawilisha kwa lugha hiohio. Hivyo, wanapoingilia uwasilishaji wa wahadhiri wao huwa ni kitendo cha hiari na dhihirisho kamili kuwa kuna upungufu fulani katika mfumo kwa mujibu wa maoni ya wanauamilifu.

Vilevile, katika taasisi za kiufundi za kitaifa, kama taasisi nyingine za elimu, wanafunzi hukabiliwa na changamoto mbalimbali; changamoto ambazo zinaweza kuwa za kijamii, kiuchumi na kisaikolojia. Ili kupambana nazo wanafunzi na wahadhiri wao walidokeza kuwa lugha ya Kiswahili hutekeleza jukumu muhimu hasa katika uwanda wa ushauri nasaha. Ilionekana jukumu hili lilikuwa la umuhimu mkubwa kwa wanafunzi kwa sababu lilikuwa la pili na asilimia 20.71 (n=29) walilichangamkia miongoni mwa wasailiwa 140. Ijapokuwa mtafiti hakupata nafasi ya kuwauliza wanafunzi na wahadhiri wao kwa nini washauri nasaha walipendelea lugha ya Kiswahili wakati wa kuwahudumia wateja wao, alihitimisha kuwa, huenda ikawa ni lugha iliyowaleta karibu na wateja wao. Mbori (2008) katika utafiti wake, aligundua kuwa lugha ya Kiswahili ilileta maridhiano nchini Rwanda baada vita vya kikabila. Wanyarwanda wengi walichagua Kinyarwanda huku kikifuatwa na lugha ya Kiswahili licha ya kuwa lugha ya Kiingereza au Kifaransa ndizo zilikuwa na wazungumzaji wengi wakati huo zikilinganishwa na Kiswahili. Ijapokuwa majukumu yanayotekelezwa na Kiswahili katika mtaala, familia ya taasisi za kiufundi za kitaifa inaonekana kufikia sasa imekumbatia na kukubali lugha ya Kiswahili.

Kando na majukumu tajwa ya Kiswahili hapo juu, lugha ya Kiswahili pia ilitumika kwa mapana katika mijadala ya wanafunzi iliyolenga mitihani ya ndani na ya kitaifa ya KNEC (*Kenya National Examinations Council*). Mijadala hii huwajenga kifikira, kiakili, na huwaleta pamoja. Barnard et al. (2004) wakimnukuu Brown ambaye alikuwa mwanaathropolojia wanasema:


> Ikiwa kwa mfano, kikundi cha watu huonekana, mara kwa mara, wakivuta mtemba kimajumui, zoezi husika linaweza kuwa kishajiisho cha kuwaleta pamoja au kuunganisha kikundi husika kuwa jamii na kuwamotisha kuwa na maadili ya urafiki na muungano (uk. 15).

Kwa mujibu wa wanauamilifu, miungano hii ya makundi inayodokezwa na Barnard na wenzake (2004) hutekeleza dhima kuu katika ustawishaji na ujenzi wa muungano miongoni mwa wanafunzi licha ya jukumu la kielimu la mijadala ya kiakademia wanapoendelea kujiandaa kwa mitihani; iwe ni ya ndani au ya kitaifa. Mijadala hii miongoni mwa wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa hutumia lugha ya Kiswahili badala ya Kiingereza, ambayo ndiyo lugha ya ufundishaji. Hili sio jambo la kushangaza kama inavyodokezwa na Senkoro (2005) ambaye aligundua kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu na sekondari walitumia Kiswahili katika mijadala yao ya kiakademia japo Kiingereza ndiyo lugha ya ufundishaji. Matokeo haya yanaoana na ya Dalvit (2004) aliyegundua kuwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Fort Hare, Afrika Kusini walitumia Isixhosa katika mijadala yao ya kiakademia. Hivyo, wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa sio tofauti na wa Chuo Kikuu cha Fort Hare wanapotumia lugha ya Kiswahili katika mijadala yao ya kiakademia badala ya lugha ya Kiingereza. Jukumu hili ni kijalizo cha utekelezaji wa mtaala wa elimu ya taasisi za kiufundi na kwa hali hii kudhihirisha umuhimu wa Kiswahili katika elimu ya taasisi za kiufundi za kitaifa.

Lugha ya Kiswahili hufundishwa wanafunzi wa astashahada katika taasisi za kiufundi za kitaifa ili kuhimilisha kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii katika mtaala wa elimu, hata hivyo ufundishaji wake ni wa kipembezoni. Hii ni kwa sababu wanafunzi

hawatahiniwi katika somo hili kama masomo mengine. Japo lugha ya Kiswahili hufundishwa katika kiwango cha astashahada, na kushirikishwa katika mtaala wa elimu ya taasisi za ufundi za kitaifa, asilimia 10.71 (n=15) miongoni mwa wasailiwa 140, waliiorodhesha ya nne kwa umuhimu. Utafiti ulionelea ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaosoma kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii ulikuwa ni mwelekeo mzuri. Hata hivyo, kozi nyingine zaidi zinapaswa kufundishwa Kiswahili na ikiwezekana wanaochukua kozi hizi wafundishwe Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Asilimia 15.71 (n=22) ya wasailiwa 140 ilionyesha lugha ya Kiswahili ilifaa zaidi kama lugha ya utoaji huduma uwandani. Hivyo, walihisi kuwa, lugha ya Kiswahili ingefanywa lugha ya utoaji huduma kwa wateja wao baada ya kufuzu na kutumwa uwandani kufanya kazi.

Dhima nyingine zinazotekelezwa na Kiswahili ingawa zinamwelekeo wa kijamii ni pamoja na mikutano isiyo rasmi miongoni mwa wanafunzi (6.43%,n=9), mazungumzo yasiyo rasmi baina ya wanafunzi na wafanyakazi mhimili (5.00%,n=9), mahubiri wakati wa kesha (4.29%,n=6), mazungumzo ya kijamii baina ya wanafunzi na wahadhiri wao (1.43%,n=2) na mawasiliano ya simu (1.43%,n=2). Kwa upande mwingine, asilimia 4.29% (n=6) ndiyo iliona kuwa lugha ya Kiswahili haikuwa na umuhimu wowote katika elimu ya kiufundi katika taasisi za kiufundi za kitaifa. Waaidha, utafiti huu uligundua kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo ilikuwa kipenzi cha mawasiliano miongoni mwa wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa. Wasailiwa waliulizwa wataje lugha ambayo wangependelea kuitumia miongoni mwao na matokeo yake yanawasilishwa katika kielelezo cha 2 kifuatacho.




**Kielelezo 2: Lugha ya Mawasiliano Miongoni mwa Wanafunzi**

Kielelezo cha 2 juu kinaonyesha lugha ya mawasiliano miongoni mwa wanafunzi katika taasisi za kiufundi za kitaifa. Ni wazi kuwa asilimia 76.06 (n=108) ya wasailiwa walionyesha kutumia lugha ya Kiswahili wakati wa kujiliwaza. Hata hivyo, asilimia 22.54 (n=32) walipendelea Kiingereza, ilhali asilimia 1.41 (n=2) walipendelea kutumia lugha za kijamii. Hivyo, wanafunzi wengi walitumia lugha ya Kiswahili kwa hiari. Utafiti huu unashadidia utafiti wa Mohochi (2005) uliogundua kuwa wanafunzi wa shule za sekondari walikuwa wakilazimishwa kuwasiliana kwa Kiingereza, hata hivyo walichagua kuwasiliana kwa Kiswahili kwa hiari bila kujali matokeo yake kutoka kwa walimu. Udhibiti wa matumizi ya Kiswahili miongoni mwa wakenya haukuanza jana kwani unaweza kufuatiliwa hadi nyakati za ukoloni (Mohochi, 2005; Nyandwaro, 2015), na huenda ikawa ndio sababu Chiraghdin na Mnyapala (1977) walifananisha Kiswahili na mti wa "mtondo" ambao hauozi wala kuzama hata ukizamishwa katika kina kirefu. Hubakia ukielea kama ilivyo katika taasisi za kiufundi za kitaifa ambapo Kiswahili katika maeneo ya pembeni katika mtaala wa elimu ya taasisi hizi. Kimsingi, maoni ya wanafunzi wa taasisi za ufundi hudhihirisha katika matendo na usemi wakati wanapoipatia nafasi katika ufafanuzi wa dhana

gumu, ushauri nasaha, mijadala ya kiakademia na kuikaribisha katika utoaji wa huduma; yote yakiwa yamefungwa katika shuka moja ya mtalaa wa elimu katika taasisi za kiufundi za kitaifa.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Utafiti huu, kwa ujumla, ulichunguza maoni ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuhusu nafasi au umuhimu wa lugha ya Kiswahili kwa elimu ya kiufundi. Walikuwa na maoni kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwa ya umuhimu mkubwa katika kuhimilisha shughuli za kiakademia na kijamii katika taasisi. Baadhi ya majukumu ya kiakademia ni pamoja na kupambanua dhana gumu, utoaji wa ushauri nasaha, utoaji wa huduma kwa walio uwandani, mijadala ya kiakademia miongoni mwa wanafunzi na pia kufundishwa kwa kiwango cha astashahada ili kuhimili kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii. Katika masuala ya kijamii hutumika kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa wanafunzi, wahadhiri wao na wafanyakazi mhimili. Halikadhalika, wanafunzi huitumia katika mikutano ya injili na mikutano isiyo rasmi. Kwa ujumla, na kwa mujibu wa wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa, lugha ya Kiswahili hutekeleza dhima kuu pembezoni mwa mtaala wa elimu ya taasisi hizi ndiposa mielekeo yao ni chanya kuihusu.

**Mapendekezo:** Utafiti huu ulinuia kuchunguza umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya. Iligundulika kuwa licha ya lugha ya Kiingereza lugha ya ufundishaji na kutekeleza jukumu rasmi katika mtaala wa elimu ya kiufundi, lugha ya Kiswahili ilihimilisha na kutia nyama mawasilisho ya wahadhiri katika masomo mbalimbali wakati wa kufafanua dhana tata kwa wanafunzi wao. Vilevile, ilitumika katika utoaji wa ushauri nasaha wakati wa kutatua shida za kijamii miongoni mwa wanafunzi. Ni kutokana na uelewa huu; utafiti huu unapendekeza kwa Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia (MOHEST) ikishirikiana na Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala (KICD) kuona jinsi wangeanzisha ufundishaji wa somo la lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wote wa taasisi za Kiufundi. Vilevile, pana haja ya kuwatahini wanafunzi wa astashahada wanaofundishwa somo la lugha ya Kiswahili wanaosoma kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi Jamii. Pia, kando na wanafunzi wa astashahada wanaosoma Kiswahili, wengine wanaosoma kozi nyingine zenye mketo wa utoaji huduma wanahitaji kufundishwa somo la lugha ya Kiswahili. Kozi hizi ni pamoja na Usimamizi wa Biashara, Mauzo na Masoko, Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii, Usimamizi wa Vyama vya Ushirika, Ununuzi na Usambazaji, Teknolojia ya vipimo vya Matibabu, Teknolojia Sayansi ya Maabara, Kilimo cha Kawaida, Ufundi Umeme, Mitindo ya Nguo na Ushonaji, Usimamizi wa Msururu wa Usambazaji, Ususi na Tiba ya Urembo na Usimamizi wa Wafanyakazi. Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia (MOHEST) inaweza kuanzisha utumiaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya ufundishaji katika kiwango cha astashahada kama ilivyo Tanzania. Zaidi ya haya, watafiti wa baadaye wanaweza kuchunguza mielekeo ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi kuhusu Kiswahili kikiwa lugha ya utoaji huduma uwandani.

## MAREJELEO


Barnard, A., Burgess, T., & Kirby, M. (2004). *As Level and A Level: Sociology*. Cambridge University Press.

Biton, T., Bonnett, K., Jones, P., Lawson, T., Skinner, D., Stanworth, M., & Webster, A. (2002). *Introductory Sociology* (4th ed.). Palgrave Macmillan.

Chiraghdin, S., & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Oxford University Press.

Dalvit, L. (2004). *Attitudes of Isixhosa-Speaking Students at the University of Fort Hare towards the Use of Isixhosa as a Language of Learning and Teaching (LOLT)* (Master's thesis). Rhodes University, Grahamstown, South Africa.

Eshleman, J. R., Cashion, B. G., & Basirico, L. A. (1993). *Sociology: An Introduction* (4th ed.). Harper Collins College Publishers Inc.

Habwe, J. (2009). The Role of Kiswahili in the Integration of East Africa. *The Journal of Pan African Studies*, 2(8), 2-10.https://www.researchgate.net/.../267949122_The_Role_of_Kiswahili_in_the_Integrat.

Ipara, I., & Mbori, B. (2009). The Role of Kiswahili in Enhancing the Potential of Science and Technology. *The Journal of Pan African Studies*, 2(8), 139-150.

Kalindimya, J. (2004). *Nafasi ya Kiswahili katika Utandawazi*. http://www.ippmedia.com/nipashe/2004/10/28/23295.html.

Kandagor, M. (2014). Nafasi ya Kiswahili katika ushirikiano wa Afrika Mashariki. Katika Michira, N., Iribemwangi, P. I., & Mbatiah, M. (Wah.), *Ukuzaji wa Kiswahili: Dhima na Majukumu ya Asasi Mbalimbali,* 180-192. Focus Publishers Ltd.

Keiko, T. (2014). Kiswahili katika kuunganisha Japani na Afrika Mashariki: Maoni ya mhadhirikutoka Chuo Kikuu cha Osaka. Katika Michira, N., Iribemwangi, P. I., & Mbatiah, M. (Wah.), *Ukuzaji wa Kiswahili: Dhima na Majukumu ya Asasi Mbalimbali,* 231- 240. Focus Publishers Ltd.

Kiango, J. G. (2002). *Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Jamii Mpya Afrika Mashariki*. http://www.qucosa.de/fileadmin/data/qucosa/documents/10082/9_12_kiango.pdf.

Kihore, Y. M. (1983). Nafasi ya Kiswahili barani Afrika. (Masoko, D. L. W., & J. S. Mdee.Whr.). *Makala ya MULIKA*, 15, 32-39.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., Hokororo, J. I. (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo.* TUKI.

Mbori, B. J. O. (2008). *The Interface between Language Attitudes and Language use in a Post-Conflict Context: The Case of Rwanda*. (Doctoral thesis, University of South Africa (UNISA), Pretoria, South Africa). http://uir.unisa.ac.za/bitstream/handle/10500/1733/thesis.pdf?sequence=1.

Mohochi, E. (2005). *Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu Lugha ya Kiswahili na Athari zake Katika Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili wa Kidato cha Nne katika Mikoa ya Pwani na Nyanza, Kenya.* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu). Chuo Kikuu cha Egerton, Kitivo cha Sanaa Sayansi Jamii, Njoro, Kenya.

Mukuthuria, M. (2006). Kiswahili and its Expanding Roles of Development in EastAfricanCooperaion: A case of Uganda. *Nordic Journal of African Studies*. http://www.njas.helsinki.fi.

Mwaliwa, C. M. (2014). Nafasi ya Kiswahili sanifu katika stesheni za televisheni nchini Kenya. Katika Michira N., Iribemwangi, P. I., & Mbatiah, M. (Wah.), *Ukuzaji wa Kiswahili: Dhima na Majukumu ya Asasi Mbalimbali*, 156-169. FocusPublishers Ltd.

Nyandwaro, K. L. (2015). *Mielekeo ya Wafanyakazi kuhusu Kiswahili kama Lugha Rasmi katika Wizara za Serikali Nchini Kenya: Mintarafu, Kaunti ya Kisii*. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kitivo cha Sanaa na Sayansi Jamii, Nairobi, Kenya.

Payne, N. (2014). Seven reasons to pay attention to the Swahili language. *Africa Business Insight*. https://www.howwemadeitinafrica.com/seven-reasons-to-pay-attention- to-the swahili-language/36057/.

Senkoro, F. E. K. (2005). *Language of Instruction: The Forgotten Factor in Education Standards in Africa?* http://www.codesria. org/IMG/ pdf/ senkoro.pdf.

Trudgill, P. (1974). *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society*. Penguin Group.

Webb, V., & Kembo-Sure. (2000). The Language of Africa. In Webb, V., & Kembo-Sure (Eds.). *African Voices: An Introduction to the Languages and Linguistics of Africa,* 26-54. Oxford University Press South Africa.